M11/1/A1SWA/SP2/SWA/TZ0/XX

22110300

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 2**
**SWAHILI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 2**
**SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 2**

Monday 16 May 2011 (morning)
Lundi 16 mai 2011 (matin)
Lunes 16 de mayo de 2011 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3e partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2e partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3e partie n'obtiendront pas une note élevée.
- Vous n'êtes pas autorisé(e) à amener des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d'examen.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.
- No se permite traer a la sala de examen copias de las obras estudiadas.


© International Baccalaureate Organization 2011

*Jibu swali* ***moja*** *tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi za sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo ambao umejitayarisha nao. Majibu ambayo* ***hayana*** *mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3* ***hayatapewa*** *alama nyingi.*

**Tamthilia**

**1.** Kila mtunzi wa kazi za fasihi anatumia mifumo na mbinu tofauti za utunzi. Kwa kuzingatia kazi mbili za waandishi wawili wa kazi za tamthilia, jadili kwa mapana na marefu mbinu wanazozitumia ukitoa mifano mwafaka, huku ukionyesha vile wanavyofaulu katika kutekeleza wajibu huu.

**2.** Tamthilia nyingi huonyesha sifa za kuaminiana, kusameheana, kujitoa kafara na kuungana katika jamii. Jadili kauli hii ukizingatia kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili tofauti ulizozisoma na uonyeshe jinsi waandishi wanavyofaulu katika kukuza sifa hizi.

**Riwaya**

**3.** Ukizingatia kazi mbili za waandishi tofauti ulizozisoma, jadili huku ukitoa mifano jinsi na kwa kiasi kipi dhana ya ukataji tamaa inavyochangia katika kukuza kazi zao.

**4.** Fasihi ni sanaa inayowasilisha hali ya maingiliano kati ya binadamu na mazingira yake. Onyesha kwa kuzingatia kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili tofauti ulizozisoma jinsi waandishi wanavyofaulu katika kuoanisha maswala haya.

**Ushairi**

**5.** Jadili kwa mapana na marefu vile methali na jazanda zinatumika katika kukuza na kuendeleza maudhui katika kazi mbili za ushairi zilizoandikwa na washairi wawili tofauti ulizozisoma.

**6.** Jadili vile wanashairi wanavyotumia mashairi kama njia moja ya kuhakiki ukandamizaji wa kijamii na wanavyofaulu katika kutekeleza kauli hii. Rejerea kazi mbili ulizojitayarishia kutoka kwa watunzi wawili tofauti.

**Riwaya za mapenzi**

**7.** Kwa kuzingatia kazi za waandishi wawili tofauti ulizojitayarishia, jadili jinsi migogoro tofauti ya kimapenzi inavyojitokeza na athari zake katika jamii.

**8.** Mapenzi huleta raha, kuvunjika kwa moyo na ukataji tamaa. Ukizingatia angalau kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili tofauti, jadili athari za maswala haya katika uandishi.

**Maswala ya ujumla**

**9.** Ukizingatia kazi mbili kutoka kwa angalau waandishi wawili ulizojitayarishia, onyesha vile waandishi wanavyotuangazia na kutuelekeza kuhusu itikadi na mitazamo tofauti ya kimaisha iliyojitokeza nyakazi zao na vile inavyochangia katika kukuza maudhui yao.

**10.** Onyesha huku ukizingatia kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili tofauti ulizozisoma vile mbinu rejeshi au mpangilio wa vitushi unavyokuzwa na waandishi hawa tofauti na uonyeshe jinsi unavyofanikisha kazi zao.

**11.** Jadili vile fasihi inavyochangia katika kutoa uhalisia wa kimaisha na jinsi uhalisia huu unavyooanishwa na sifa za wahusika kwenye kazi zao. Zingatia angalau kazi mbili za waandishi wawili tofauti ulizojitayarishia.

**12.** Jadili jinsi dhana ya ushujaa inavyokuzwa katika kazi mbili kutoka kwa waandishi wawili uliojitayarisha, na uonyeshe kama nyezo walizozitumia waadishi kukuza dhana hii ni za haki na ukweli.

---